JIMBO KATOLIKI LA GEITA
UTARATIBU WA IBADA ZA JUBILEI YA MI-AKA 25 YA JIMBO NA KUTABARUKU KANISA KUU LA JIMBO

Tar 25—26 Septemba 2010

SHUKRANI

Kamati ya Liturjia inatoa shukrani kwanza kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha kuandaa utaratibu wa Ibada na kutoa kitabu hiki. Kamati vilevile inamshukuru Baba Askofu Damian D. Dallu wa jimbo letu la Geita kwa ushauri wake juu ya utaratibu wa ibada hizi. Kamati inalo deni la kuwashukuru kwa namna ya pekee Baba Askofu Salutaris Libena Askofu msaidizi wa Jimb kuu la Dar Es salaam na Monsinyori Kangalawe kwa ushauri wao wa kiliturjia katika kufanikisha kazi hizi.

Tunamshukuru pia Padre Thobias Kuzenza (Mkurugenzi wa Liturjia jimboni Geita) kwa maelekezo yake mazuri.

Hatuwezi kuwataja wote walioshrika katika kazi hii ila tunamwombea kila mmoja baraka za Mwanyezi Mungu katika utume wake.

Mungu Awapariki sana.

Padre Francis Bonamax Muganyizi
(Kwa niaba ya Kamati Ya Liturjia)

YALIYOMO

Ibada ya Masifu ya Jioni…….4

Ibada ya Misa ya Kutabaruku kanisa kuu la Jimbo…14

SEHEMU YA KWANZA
Ibada ya Mwanzo……...14
Mbele ya kanisa kuu…….…..18
Baraka ya maji na kunyunyiza……...20

SEHEMU YA PILI
Liturjia ya Neno…….……22

SEHEMU YA TATU
Sala rasmi ya kutabaruku na mpako……..26

SEHEMU YA NNE
Liturjia ya Ekaristi……..…...……33

IBADA YA MWISHO……..…..…...45

MASIFU YA JIONI (VIJILIA)
TAREHE 25/9/2010
KAWAIDA KWA KUTABARUKIWA KANISA.
MASIFU YA JIONI 1

UTENZI.

Msingi mmoja tu wa Kanisa
Ni Yesu Kristu, wake Bwana;
Kanisa ndio kwanza kaliumba
Kwa maji na kwa neno kutamka:
'Toka mbinguni kaja litafuta
Liwe mke wake Mtakatifu,
Kwa damu yake alilinunua;
Kwa 'jili ya uzima wake kafa.

Katwaliwa 'toka kila taifa,
Ila duniani kote ni moja,
Kanuni yake ya wokovu ndiyo:
Bwana, ubatizo, imani moja,
Lasifu jina takatifu moja;
Linashiriki chakula kimoja,
Latarajia tumaini moja
Kwa kila neema lililopata.

Ingawa kwa mshangao, dharau,
Watu waliona lakandamizwa,
Kwa mafarakano la tengwa – tengwa ,
Kwa mwingi uzushi lasumbuliwa,
Kumbe watakatifu wapo macho,
'Hata lini? kwa sauti walia;
Ndipo mara usiku wa vilio

2. Shangwe na vifijo kwa waamini wa Jimbo letu kweli Jubilei yetu
3. Tufurahi sote tumwombe Mungu atujalie kuinjilisha tena kwa wasiomjua .

NINASEMA MIMI (By M. MTIGWA)
Ninasema mimi, ninasema mimi ninasema Mwenyezi Mungu umetia furaha moyoni mwangu x2 kwa heshima nitakutukuza (Mungu wangu) tena kwa ujasiri nitasimulia matendo yako siku zote x2

1. Umeniona ukanihurumia, na kwa upole ukanisaidia nina amani na sasa najilaza napata usingizi mnono
2. Ee Bwana mimi ni kitu ngani kwako? Unitazame hata uni-kumbuke nina furaha matumaini makubwa na wanijali sikia.

Kwa kuwa kwa furaha mmetakasika, mnaweza kuwa na Mungu ndani yenu, na kuirithi heri ya milele pamoja na watakatifu wote.

Wote . **Amina.**

Askofu anatwaa bakora na kuendelea

Awabariki Mungu Mwenyezi, Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.

Wote . **Amina.**

Nyimbo za Mwisho

YAUWE BAMBE – JUBILEI (Gervase Baluhendekela)

Jublei Jubilei ya jimbo letu Geita x2
Tujalie Baba Aiya, Jubilei njema Aiya,
Mjalie Baba Aiya, Askofu wetu Aiya,
Mapidiri wote Aiya, na watawa wote Aiya,
Walei wote Aiya, na tufanye shangwe Aiya
Tuzidi kudumu katika umoja na mapendo x2

1. Kwa jubilei hii njema tunazidi kukuomba, imarisha ukristu wetu, tunazidi kukuomba. Waongoze wachungaji wetu na watawa wetu Baba wajawe kheri yako

2. Kwa jubilei hii njema tunazidi kukuomba, wajalie wazazi wote hekima na busara zako Wawalee watoto wao, maadili ya kikristu katika jamii.

NI SHANGWE (ALBERT – AGE, Nzera Parish)

Ni shangwe kwa waamini wote wa Jimbo la Geita x 2
Kwa kuadhimisha Jubilei, Jubilei ya Jimbo letu,
Jubilei ya miaka ishirini na mitano x2

1. Tumshukuru Mungu kwa zawadi ya pekee kabisa aliyotujali Jimboni mwetu

Utakuwa asubuhi wa nyimbo.

Kati ya taabu na matatizo,
Kati ya ghasia na vita vyake,
Langojea ujio na upeo,
Wa amani halisi ya milele;
Mpaka macho yake yenye hamu
Yatakapouona utukufu,
Na Kanisa kuu litaposhinda,
Ndipo Kanisa litapotulia.

Ila dunia imeungana
Na Mungu Mmoja Nafsi Tatu,
Tena kiajabu limeungana
Na waliojipatia pumziko:
Enyi wenye heri watakatifu!
Bwana, tupe neema ili nasi ,
Tulio wanyenyekevu na duni ,
Kama wao tukae nawe huko.

ZABURI

Ant. 1: Barabara za Yerusalemu zitashangilia; vinjia vyake vyote vitajaa nyimbo za furaha, aleluya.

Zab. 147: 1 – 11 (Ni vizuri kumsifu Mungu)

Ni vizuri kumuimbia Mungu wetu sifa;*
ni vizuri na sawa kabisa kumsifu.

Mungu anaurekebisha mji wa Yerusalemu.*
Anawarudisha salama wakimbizi wake.

Anawaponya waliovunjika moyo;*
anawatibu majeraha yao.

Ameweka idadi ya nyota ,*
na kuzipa kila moja jina.

Bwana wetu ni mkuu, ana nguvu nyingi;*
Maarifa yake hayana kipimo.

Mungu huwakweza wanyenyekevu,*
lakini huwatupa waovu mavumbini.

Mwimbieni Mungu nyimbo za shukrani,*
mpigieni kinubi Mungu wetu!

Yeye alifunika anga kwa mawingu, /
huitengenezea dunia mvua,*
na kuchipuza nyasi vilimani.

Huwapa wanyama chakula chao,*
na kulisha makinda ya nguruwe wanaolia.

Yeye hapendezwi na nguvu za farasi,*
wala hafarijiki na ushujaa waaskari;

lakini hupendezwa na watu wamchao
watu wanaotegemea upendo wake mkuu.

Ant. 1: Barabara za Yerusalemu zitashangilia; vinjia vyake vyote vitajaa nyimbo za furaha, aleluya.

exorantes;
Ut qui petentibus desiderata concedis, eosdem non deserans, ad praemia futura disponas.
Per Christum Dominum nostrum.

R. **AMEN**

BARAKA NA KUAGA

Askofu anavaa mitra na kusema

Askofu: **Bwana awe nanyi.**
Wote: **Awe pia nawe.**

Hapo shemasi, kadiri ya kufaa, awaalike watu wote kwa maneno haya au mengine yafananayo:

Inamisheni vichwa kupata baraka

Kisha Askofu anawawekea mikono watu kuwabariki akisema:

Bwana wa mbinguni na dunia amewakusanya leo
mpate kuitabaruku nyumba hii,
Yeye mwenyewe awajaze, neema tele za mbinguni.

Wote . **Amina.**

Askofu:

Yeye aliyetaka kuwakusanya katika Mwanae watu wote waliotawanyika, awajalie kuwa hekalu na makao ya Roho Mtakatifu.

Wote . **Amina.**

Askofu:

Patrem /immensae majestatis.
Venerandum tuum verum / et unicum filium
Sanctum quoque / Paraclitum spiritum
Tu Rex gloriae christe.
Tu Patris / sempiternus es filius.
Tu ad liberandum susceptuus hominem / non horruisti virginis uterum.
Tu devicto mortis acculeo / aperuist credentibus regna caelorum.
Tu ad dexteram Dei sedes / in gloria Patris
Judex crederis / Es se venturus .
Tu ergo quaesumus, tuis famulis subveni / quos pretioso sanguine redemist.
Aeterna fact / cum sanctis tuis in gloria numerari.
Salvum fac populum tuum domine / et benedic hae reditatuae
Et regeos / et extolle illos / usque ae in aeternum.
Per singulos dies / benedicimus te.
Et laudamus nomen tuum in saeculum / et saeculum saeculi.
Dignare Domine die isto / sine peccato nos custodire.
Miserere nosri Domine / Miserere nostri.
Fiat misericordia tua Domine Super nos /
quemadmodum speravimus in te.
In te Domine speravi / non confundar in aeternum.

V. Benedicamus Patrem, et Fillum cum sancto Spiritu.
R. Laudemus et superexaltemus eum in saecula.
V. Benedictus es Domine, in firmamento coeli.
R. Et laudabilis, et gloriosus, et superexaltatatus in saecula.
V. Domine exaud ortionem meam.
R. Et clamor meus ad te veniat..
V. Dominus vibiscum.
R. Et cum spiritu tuo.

OREMUS,

Deus, cujus misericordia non est numerus, et bonitatis infinitus est thesaurus;
Piissimae majestati tuae pro collatis donis gratis agimus, tuam semper clementiam

Anti 2: Bwana anayeimarisha mapingo ya milango yako , amewabariki watoto walio ndani yako (aleluya)

Zab. 147:12 – 20 (Ni vizuri kumsifu Mungu)

Ee Yerusalemu, umsifu Mungu!*
Umsifu Mungu wako,ee Sion!

Maana ameimarisha milango yako,*
amewabariki watu waliomo kwako.

Ameweka amani mipakani mwako;*
anakushibisha kwa ngano safi kabisa.

Yeye hupeleka amri yake duniani,*
na Neno lake hutekelezwa upesi.

Hutandaza theluji kama pamba,*
hutawanya umande kama majivu.

Huleta nvua ya mawe /
- vipande vikubwa vikubwa kama mkate - *
Na kwa ubaridi wake maji huganda.

Kisha hutoa amri, na maji hayo huyeyuka;*
Huvumisha upepo wake, nayo hutiririka.

HumjulishaYakobo ujumbe wake,*
na Israeli amri na maagizo yake.

Anti 2: Bwana anayeimarisha mapingo ya milango yako , amewabariki watoto walio ndani yako (aleluya).

Ant. 3: Watakatifu, waliokutanika katika mji wa Mungu, wanafurahi; malaika wanaimba mbele ya kiti cha enzi cha Mungu aleluya.

WIMBO (Rej Ufu. 19:1,2,5 – 7)

Aleluya.
Wokovu, utukufu na nguvu ni mali yake Mungu wetu! *
(W. Aleluya.)

Maana hukumu yake ni ya kweli na ya haki.
W. Aleluya (aleluya).

Aleluya.
Msifuni Mungu, enyi watumishi wake wote ,*
(W. Aleluya.)

Nanyi nyote mnaomcha, wadogo kwa wakubwa.
W. Aleluya (aleluya) .

Aleluya.
Bwana Mungu mwenyezi, ni Mfalme!*
(W. Aleluya.)

Tufurahi na kushangilia, tumtukuze.
W. Aleluya (aleluya) .

Wote . **Amina.**

Maandamano kuelekea tabernakulo

NDIYO MKATE WA MALAIKA (J MAKOYE).
Ndiyo mkate wa Malaika, chakula cha wasafiri wenye raha ya milele siyo mkate wa kafiri x2

1. Alhamisi Yesu mwokozi alisema kwa sauti huu ndiyo mwili wangu haya maneno magumu.
2. Vilevile mwokozi wetu alisema kama mwanzo hii ndiyo damu yangu, fanyeni hivyo daima.
3. Vyote ni kwa ajili yetu, ni kwa ajili ya wote kwa ondoleo la dhambi twatubu makosa yetu.

KUSHUKURU

BWANA ASANTE (By OCTAVIAN MICHAEL)
Bwana asante sana twakushukuru kwa mema yako asante x2

1. Umetulisha mwili wako asante Bwana asante
2. Umetunywesha damu yako asante Bwana Asante
3. Umetulisha chakula cha mbinguni asante Bwana asante.

Wote tusimame

TE DEUM.
Te deum laudamus, te Dominum confitemur.
Te aeternum Patrem / omnes terra veneratur.
Tibi omnes Angeli / tibi caeli et unversae potestates
Tibi cherubim et seraphim / incessabili voce proclamant.
Sanctus, Sanctus, Sanctus Dominus Deus sabaoth.
Pleni sunt caeli et terra / majestatis gloriae tu ae.
Te gloriosus / Apostolorum chorus.
Te prophetarum / laudabilis numerus.
Te martyrum / cadidatus / laudat exercitus.
Te per orbem terrarum / sancta confitetur Ecclesia.

kwa heshima, tusogee tukale mwili wa Bwana.

2. Ndicho chakula cha kweli tukale mwili wa Bwana, kinachotoka mbinguni, tukale mwili wa Bwana.
3. Chakula safi cha roho tukale mwili wa Bwana daima atushibisha tukale mwaili wa Bwana.

YESU WANGU NAJITOLEA (PD. M. MWANAM-PEPO)

1. Yesu mwema najitolea kwako kwa leo hii na siku zote, nafsi yangu na moyo wangu wote (heri kweli heri kweli raha ya uwingu)x 2
2. Ndani mwangu umekuja daima, kuwa nami ni pendo lako, Ewe mpenzi mwenye utamu mwingi (ni mapendo ni mapendo ya moyo wako) x 2
3. Nitaweza kushuhudia nini kwa wema huu na pendo lako, roho yangu, umenifadhilia

(nikupende nikupende nikupende ni tamu yangu) x2

UFUNGUZI WA KIKANISA CHA SAKRAMENTI KUU

Sala Baada ya komunyo

TUOMBE:

Ee Bwana, tunakuomba utujalie tuelewe vema zaidi mafundisho yako kwa njia ya sakramenti takatifu tuliyoipokea;
Tuweze kukuabudu siku zote za katika hekalu lako takatifu .
Hatimaye tukakutukuze mbinguni pamoja na Wata-katifu wote. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.

Aleluya.
Wakati wa arusi ya mwana - kondaoo umefika,*
(W. Aleluya.)

Na Bibi arusi yuko tayari.
W. Aleluya (aleluya) .

Ant. 3: Watakatifu, waliokutanika katika mji wa Mungu, wanafurahi; malaika wanaimba mbele ya kiti cha enzi cha Mungu aleluya.

SOMO Ef. 2:19 – 22
Ninyi si wageni tena, wala si watu wa nje; ninyi ni raia pamoja na watu wa Mungu, na ni watu wa jamaa ya Mungu. Mmejengwa juu ya msingi uliowekwa na mi-tume na manabii, naye Kristo mwenyewe ndiye jiwe kuu la msingi. Yeye ndiye mwenye kulitengeneza jengo lote, na kulikuza hata liwe hekalu takatifu kwa ajili ya Bwana. Katika kuungana naye, ninyi pia mnajengwa pamoja na wote, wengine muwe makao ya Mungu kwa njia ya Roho wake.

KIITIKIZANO
K. Nyumba yako, Bwana imeteuliwa. Inatambulikana kwa utakatifu wake. *(W. Warudie)*
K. Kwa nyakati zote.
W. Inatambulikana kwa watakatifu wake.
K. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu.
W. Nyumba yako, Bwana imeteuliwa. Inatambulikana kwa utakatifu wake.

Ant. Ya Wimbo wa Bikira Maria:
Furahini pamoja na Yerusalemu, na ushangilieni mji huo milele, ninyi nyote mnaoupenda
(aleluya) .

WIMBO WA BIKIRA MARIA

Lk. 1: 46 – 55

Moyo wangu wamtukuza Bwana, /
Roho yangu inafurahi *
kwa sababu ya Mungu Mwokozi wangu.

Kwa kuwa amemwangalia kwa huruma /
mtumishi wake mdogo,*
hivyo tangu sasa watu wote wataniita mwenye heri.

Kwa kuwa Mwenyezi Mungu amenitendea makuu,*
jina lake ni takatifu.

Huruma yake kwa watu wanaomcha*
hudumu kizazi hata kizazi.

Amefanya mambo makuu kwa mkono wake:*
amewatawanya wenye kiburi katika mawazo ya mioyo yao;
akawakweza wanyenyekevu.

Wenye njaa amewashibisha mema,*
Matajiri amewaacha waende mikono mitupu.

Amempokea Israel mtumishi wake,
akikumbuka huruma yake,

yangu iko radhi fanya yote utakayo.

2. Unitilie bidii moyoni mwangu nisikie uvuguvugu nipe moto wako, fumbua macho yangu Bwana nikuone Yesu niheshimu Ekaristi chakula cha mbunguni.

NIRUHUSU YESU WANGU (E. F KIDALUSO)
Niruhusu Yesu wangu niijongee meza yako unisamehe dhambi mwokozi uje rohoni mwangu uniokoe.
Njoo kaa ndani yangu nami nikae ndani yako ili nipate amani tele, ndani ya roho yangu nifarijike.
(wewe Bwana wanijua hata nafsi mwangu wewe ndiwe tabibu pekee wa roho yangu tena ndiwe kimbilio langu x2

1. Tazama Yesu wangu naijongea karamu yako, pengine kwako Bwana sikustahili kuijongea unihurumie Ee Yesu wangu unisamehe.
2. Hakika kwako Bwana makosa mengi nimeyatenda ubinadamu wangu siwezi kuficha kwako Bwana, unihurumie Ee Yesu wangu unisamehe.

KULENI HUU MWALI WANGU (By C. NGINDU – Geita Parish)
Kuleni huu mwili wangu na pia kunyweni hii ni damu yangu x2
Heri yao walioalikwa kwa karamu ya Bwana x2

1. Yesu aliketi chakulani na mitume wake pamoja. Akatwaa mikononi mwake mkate na divai, akabariki akamega akawapa mitume wake.
2. Yeye alaye huu mwili wangu na kuinywa damu yangu, atakaa ndani yangu, mimi pia ndani yake, naye atakuwa mzima siku zote hata milele.

TWENDE TUKALE MWILI (FR.BULALA, M.)
Twende tukale mwili wake Bwana x2
Tupate uzima wamilele twende tukale mwili wake Bwana x2

1. Yesu yupo Altareni mkale mwili wa Bwana

Hata milele.

Askofu:
Ee Bwana Yesu Kristo uliyewaambia Mitume wako:
Nawaachieni amani, nawapeni amani yangu:
Usizitazame dhambi zetu, ila tu imani ya Kanisa lako:
Ulijalie amani na umoja kama yalivyo mapenzi yako.
Unayeishi na kutawala, daima na milele.

Wote: Amina.

MWANAKONDOO (AGNUS DEI)
Agnus Dei, qui tollis peccata mundi;
Miserere nobis.
Agnus Dei, qui tollis peccata mundi;
Miserere nobis.
Agnus Dei, qui tollis peccata mundi;
Dona nobis pacem.

Askofu anainua Mwili wa Kristu akisema
Huyu ndiye Mwana kondoo wa Mungu aondoaye dhambi za dunia.
Heri yao walioalikwa kwenye karamu ya Bwana.

Wote: Ee Bwana, sistahili uingie kwangu,
Lakini sema neno tu na roho yangu itapona.

Nyimbo za komunyo
ONJENI MUONE (VIANNEY S. GALLUS - Mwangika Parish)
(Onjeni muone Onjeni muone Onjeni muone) x2
(Ya kuwa Bwana ni mwema) x2
Onjeni muone ya kuwa Bwana ni mwema) x2

1. Yesu wangu Mungu wangu kaa pamwe nami, Ee Bwana kila wakati na kila saa nipe furaha matumaini moyoni mwangu roho

Kama alivyowaahidia wazee wetu,*
Abrahamu na uzao wake hata milele.

Furahini pamoja na Yerusalemu, na ushangilieni mji huo milele, ninyi nyote mnaoupenda (aleluya) .

MAOMBEZI

Tumuombe Mwokozi wetu, aliyeutoa uhai wake ili awakusanye pamoja watoto wa Mungu waliokuwa wametawanyika.

W. Bwana ulikumbuke Kanisa lako.

Bwana Yesu , aliwaamuru wanafunzi wako wasikie maneno yako na kuyatekeleza kwa vitendo;
- kila mara uliimarishe Kanisa lako katika imani , ujasiri na matumaini. (W.)

Bwana Yesu, kutoka katika ubavu wako uliotobolewa ilitoka damu na maji;
- ulifanye Kanisa lako liwe hai kweli kweli , kwa njia ya sakramenti za agano jipya na la milele. (W.)

Bwana Yesu, wewe upo kati yao wale wanaokusanyika kwa jina lako;
- ulisikie Kanisa lako, ambalo limejumuika na kusali. (W.)

Bwana Yesu, unafika na Baba kuishi ndani ya wale wanaokupenda ;

- ulikamilishe Kanisa lako ulimwenguni kote, katika mapendo yako ya kimungu. (W.)

Bwana Yesu, yeyote yule anayefika kwako harudishwi kamwe;
- uwapokee katika nyumba ya Baba yako,wale wote waliofariki dunia. (W.)

Baba Yetu uliye mbingun…....

SALA
Mungu Mwenyezi, tunapotabaruku kwa furaha nyumba yako hii, usikilize sala ya taifa lako, na utujalie ibada yetu katika Kanisa hili iwe nyofu na takatifu, ilitukuze jina lako na kutufikisha sisi kwenye utimilifu wa wokovu.
(Tunaomba hayo) kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristu Mwanao anayeishi na kutawala nawe na Roho Mtakatifu Mungu daima na milele.
Wote: Amina

K. Bwana awe nanyi
W. Awe pia nawe
K. Awabariki Mungu Mwenyezi, Baba na Mwana na Roho
Mtakatifu
W. Amina

K. Tumtukuze Bwana
W. Tumshukuru Mungu

Wote: Amina.

IBADA YA KOMUNYO
Askofu:
Na sasa tusali kwa imani
Ile sala aliyotufundisha
Bwana wetu:

Wote: Baba yetu uliye mbinguni,
Jina lako litukuzwe,
Ufalme wako ufike,
Utakalo lifanyike duniani kama mbiguni
Utupe leo mkate wetu wa kila siku,
Utusamehe makosa yetu,
Kama tunavyowasamehe na sisi waliotukosea.
Usitutie katika kishawishi,
Lakini utuopoe maovuni.

Askofu:
Ee Bwana,
Tunakuomba utuopoe katika maovu yote,
Utujalie kwa wem amani maishani mwetu.
Utuepushe daima na dhambi
Kwa huruma yako,
Tusifadhaishwe na jambo lolote.
Tungojee kwa matumaini
Kurudi kwake Mombozi wetu Yesu Kristo.

Wote: Kwa kuwa ufalme ni wako,
Na nguvu, na utukufu,

Tujazwe na Roho wako Mtakatifu,
Ili tuwe mwili mmoja na Roho moja katika Kristo.

Yeye atufanye tuwe kwako sadaka ya milele, **C_1**
Ili tuweze kupata urithi pamoja na wateule wako:
Bikira Maria mwenye heri, Mama wa Mungu,
Na Mitume na Mashahidi wako wenye heri
Na watakatifu wote,
Ambao daima wanatuombea kwako.

Tunakuomba, ee Bwana, sadaka hii ya kutupatanisha nawe **C_2**
Ilete amani na wokovu duniani kote.
Uliiimarishie Kanisa lako imani na mapendo hapa duniani,
Yaani mtumishi wako Baba Mtakatifu wetu Benedikto XVI
Na Askofu wetu Damiani Denis Dallu,
Maaskofu na watumishi wako wote,
Pamoja na taifa lako lote.

Usikilize kwa wema **C_3**
Sala za jamaa hii iliyo hapa mbele yako.
Ee Baba mwema, kwa huruma yako uwakusanye kwako
Wanao wote waliotawanyika popote duniani.

Uwapokee katika ufalme wako ndugu zetu marehemu
Na wote walioaga dunia katika hali ya neema.
Nasi tunatumaini kujawa na utukufu milele
Katika ufalme wako.

Utujalie hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu
Aliye asili ya mema yote.

Kwa njia yake, pamoja naye, na ndani yake,
Wewe Mungu Baba Mwenyezi
Katika umoja wa Roho Mtakatifu
Unapata heshima na utukufu wote,
Daima na milele.

SALVE REGINA

Salve Regina, Mater misericordiae, Vita dulcedo et spes nostra salve.
Ad te clamamus exsules filii Havae.
Ad te suspiramus, gementes et flentes in hac lacrima-rum vale.
Eia ergo advocate nostra, ilos tuos misericordes oculos ad nos converte.
Et Jesum, benedictum fructum ventris tui nobis post hoc exlium ostende. O Clemens, O pia, O dulcis Virgo Maria.

IBADA YA MISA TAKATIFU YA KUTABARUKU KANISA KUU LA JIMBO NA MAADHIMISHO YA MIAKA 25 YA JIMBO TAR 26.9.2010

SEHEMU YA KWANZA

IBADA YA MWANZO

Maandamano

1. Msalaba kati ya mishumaa miwili iwakayo
2. Wanakwaya
3. Watawa
4. Mafrateri
5. Mapadre
6. Maaskofu
7. Mashemasi
8. Askofu kiongozi wa Ibada
9. Watumishi wa kofia na fimbo

(*Maandamano yanweza kufupishwa kwa kupunguza idadi ya waandamanaji)*

NYIMBO ZA MAANDAMANO KUELEKEA MBELE YA KANISA KUU

WEWE NDIWE KUHANI. (By Hilari Msigwa, Geita Parish)

Wewe ndiwe kuhani hata milele x 5 hata milele kwa mfano wa Melkisedeki.

1. Neno la Mungu kwa Bwana wangu huketi mkono wako wa Kuume.

Huu ni mwli wangu,
Utakaotolewa kwa ajili yenu.

Vivyo hivyo baada ya kula,

Akatwaa kikombe,
Akakushukuru, akakutukuza,
Akawapa wafuasi wake akisema:

Twaeni, mnywe wote:
Hiki ni kikombe cha damu yangu,
Damu ya agano jipya la milele,
Itakayomwagika kwa ajili yenu
Na kwa ajili ya wengi
Kwa maondoleo ya dhambi.
Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi.

Hili ni fumbo la Imani:

Wote: **Ee Bwana tunatangaza kifo chako**
na kutukuza ufuffuko wako mpaka utakapokuja.

Kwa hiyo, ee Bwana, tunapokumbuka mateso ya huyo Mwanao,
Na kufufuka na kupaa kwake mbinguni;
Tunapongojea na kuja kwake mara ya pili,
Tunakutolea kwa shukrani
Sadaka hii yenye uzima na utakatifu.

Tunakuomba uiangalie na kuikubali hii sadaka ya Kanisa lako
Uliyotaka kutulizwa nayo.
Utajalie sisi tunalolishwa Mwili na Damu ya Mwanao

Pale ambapo wewe utakuwapo kwa karne zote katika wote ,
Bila mwisho wa Kristo Mwanga wa kweli atang'aa kwa daima.

Ee Bwana, kwa njia yake, pamoja na malaika na Watakatifu wote tunakuungama tukisema kwa shangwe:

MTAKATIFU (SANCTUS)
Sanctus, Sanctus, sanctus / Dominus Deus Sabaoth. /
Pleni sunt caeli et terra gloria tua. / Hosana in excelsis. /
Benedictus qui venit in nomine Domini, / Hosana in excelsis.

SALA YA EKARISTI YA III

Ee Bwana kweli u mtakatifu,
Na kila kiumbe kilichoumbwa nawe kinakusifu kwa haki.
Maana, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristu Mwanao,
Na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu unatia uzima na kutakasa vitu vyote,
Wala huachi kuwakusanya watu kwako,
Ili toka mawio ya jua hata machweo yake wakutolee sadaka safi

Basi, tunakusihi, Ee Bwana,
Uzibariki dhabihu hizi tunazokutolea
Upende kuzitakasa kwa Roho wako
Ili zigeuke kuwa Mwili na + Damu
Ya Mwanao Bwana wetu Yesu Kristu
Aliyetuamuru tuadhimishe mafumbo haya.

Usiku ule alipotolewa
Yeye mwenyewe alitwaa mkate
Akashukuru akakutukuza,
Akaumega, akawapa wafuasi wake, aksema:

Twaeni mle wote:

2. Hata niwafanyapo adui zako, niwawekapo chini ya miguu yako
3. Bwana atainyosha toka Sayuni atainyosha fimbo ya nguvu zangu
4. Wewe ndiwe kuhani hata milele, kwa mfano wa Melkisedeki.

MAKASISI NA WATAWA NA WALEI WOTE (By Albert AGE Nzera Parish)
Makasisi na watawa na walei wote wa Jimbo la Geita,
Njooni tufanye tafakari ya Jubilei yetu x 2
Kwani tunaadhimisha Jubilei ya miaka ishini na mitano
Njoni tutafakari tena tumshukuru Mungu x2

1. Tumwombe Mungu baba atujalie Jubilei, Njema katika familia
za waamini wote.
2. Mungu Baba Mwenyezi umjalie Askofu wetu, moyo wa
Uchungaji kwa jumuiya yake.
3. Na wachungaji wetu uwatie Baraka zako ee Bwana,
Waliongoze vema kanisa lako lote

SHANGWE YA JUBILEI (Evarist Enock Geita Parish)
Shangwe nderemo na na chereko na vifujo ni vya nini?
Jubilei ya miaka ishirini na tano ya Jimbo,
kinababa kinamama na vijana na wageni wetu, Jubile Geita.
Umoja na mapendo katika Kristo.

Jubilei ni alama thabiti ya imani yetu inayoonyesha ukomavu wetu wa Jimbo.

1. Inatukumbusha inatukumbusha mwanzo wa Jimbo letu
   Inatuonyesha, inatuonyesha umoja wetu, umoja wetu

2. Inatuhimiza, inatuhimiza kuishi neno lake
   Inatueleza, inatueleza kupenda watu wote

3. Pia yatangaza,pia yatangaza uwepo wake Mungu
   Inaimarisha, inaimarisha na familia zetu

4. Tucheze pamoja, tuimbe pamoja tumsifu Mungu
   Ametujalia katupa baraka pia neena zake.

5. Tuishi Pamoja, Tudumu daima kwenye imani yetu
   Na tumshukuru Mungu Baba yetu leo na siku zote.

JUBILEI GEITA (Frt. Shikombe, A)

Jubilei Geita, Umoja na Mapendo katika Kristo x 2

1. Tuiadhimishe Jubilei, katika Kristo
   Tunamshukru Mungu wetu, katika Kristo
   Baba Mungu tujalie neema, katika Kristo
   Takatifu za mioyo yetu, katika Kristo

2. Tujalie roho ya utume, katika Kristo
   Simamia umisionari, katika Kristo
   Simamia Seminari zetu, katika Kristo
   Zibariki jumuiya zetu, katika Kristo.

Sala juu ya vipaji

Askofu:

Ee Bwana, dhabihu za Kanisa lako linalofurahi zikupendeze. Nalo taifa lako linapokutana katika nyumba hii takatifu, lipate wokovu usio na mwisho, kwa njia ya mafumbo haya. Tunaomba hayo kwa njia ya Kristo Bwana wetu.

Wote: **Amina**

UTAGULIZI:

P: **Bwana awe nanyi**
W. **Awe pia nawe**
P. **Inueni mioyo**
W.**Tumeinua kwa Bwana**
P. **Tumshukuru Bwana Mungu wetu**
W. **Ni vema na haki**

Kweli ni wajibu na haki,vema na vizuri sana kukushukuru wewe Baba Mtakatifu , daima na popote.

Wewe uliyetengeneza ulimwengu wote kuwa hekalu la utukufu wako ili jina lako lidhihirishwe popote,

Hata hivyo hukaa mahali panapofaa kwa ajili ya mafunbo ya kiMungu ili yatolewe kwako: ndiyo sababu nyumba hii ya sala, ilijengwa na mikono ya watu, kwa shangwe tunautabarukia utukufu wako.

Hapa fumbo la hekalu la kweli linaashiriawa,
Na sura ya Yerusalemu ya mbinguni inaonekana:
Kwa mwili wa mwanao, uliozaliwa na Mama Bikira,
Umeufanya kuwa kwako hekalu takatifu,
ambamo utimilifu wa umungu wako unakaa.
ulifanya Kanisa kuwa mji mtakatifu,
uliojengwa juu ya msingi wa Mitume, juu ya jiwe la msingi,
yaani Yesu Kristo mwenyewe.
Mawe yaliyoteuliwa na kukuzwa kwa upendo,

wanadamu nakusihi upokee sadaka yangu.

2. Ingawa ni kidogo ninaleta upokee ni juhudi yetu sisi wanadamu nakusihi upokee sadaka yangu.

3. Unyonge pia udhaifu wangu ninaleta ninaomba uzidi kunipa nguvu moyo na uwezo wa kutenda mema mengi.

HUU SASA NI WAKATI (BY MSIKE)

Huu ni wakati wa kutoa sadaka, toa kwa ukarimu ulicholeta ndugu usifiche Mungu anakuona x2

1. Sasa ni wakati awakutoa sadaka kila mtu aanze kufikiria.

2. Japo ni kidogo tutoe kwa ukarimu kutoa ni moyo wala si utajiri.

3. Ewe ndugu twende mbele ya Bwana tukatoe sadaka kwa moyo wa upendo.

Maandamano ya vipaji

NI ZAWADI ZETU (Zinza Melody)

1. Ni zawadi zetu, Baba pokea sadaka zetu tunaleta kwako twaomba uzipokee
2. Na mazao yetu, Baba pokea sadaka……..…..,,…….
3. Nazo fedha zetu, Baba pokea sadaka……..,,……..
4. Nazo nyoyo zetu, Baba pokea sadaka……..,,……..
5. Na maombi yetu, Baba pokea sadaka……..,,……
6. Na mawazo yetu, Baba pokea sadaka……..,,……...

EE BWANA IKUPENDEZE (By Nkomagu)

(*Ee Bwana ikupendezi, ikupendeze sadaka ya sikukuu hii ya leo)x 2 Sadaka hii ndiyo fidia timilifu, yakutupatanisha na wewe Mungu Baba. Na pia ibada timilifu ya kukutolea Wewe Ee Mungu wetu*

1. Tunakutolea mkate na divai kazi ya mikono yetu wanadamu twakuomba Ee Baba uvipokee.
2. Tunakutolea pia na fedha zetu, na pia mazao ya mashamba yetu, twakuomba Ee Baba uvipokee.

3. Uwalinde makuhani wetu, katika Kristo
Simamia tume za walei, katika Kristo
Tujalie moyo wenye toba, Katika Kristo
Tutamani maisha ya sala, katika Kristo

4. Amsha fadhila ya imani, katika Kristo
Tuwashie moyo wa mapendo, katika Kristo
Tujalie moyo wa umoja, katika Kristo
Tutamani na kufika kwako, katika Kristo

WAAMINI WA JIMBO LA GEITA (BY NY-ACHIHA Nzera Parish)

Waamini wa Jimbo la Geita ni shangwe, kuadhimisha miaka ishirini na tano ya Jimbo letu x2

Mbegu ya neno uliyotujalia sisi imezaa tunda lenye baraka Jimbo la Geita x 2

Tufurahie (sisi) .tushangilie (sote) tupige makofi tucheze ngoma za kikwetu, huku tukilinga, tabasamu tele.

1. Ee Mungu Mwenyezi uzibariki familia zetu ziwe chimbuko la Kanisa, kanisa lako.

2. Ubariki pia watoto wetu, na watoto wetu wawe chimbuko la Kanisa, kanisa lako.

3.Uwaimarishie na katika uadilifu wako vijana wetu wito wao wa kujituma

4.Uimarishe roho ya utume kwa walei wote wajibu wao kwa Kanisa kusimamia.

MBIU YA JUBILEI (BY J.P. MASENGA).

Jubilei Geita, Umoja na Mapendo katika Kristo x 2

Jubilei Geita Umoja na mapendo katika Kristu

Njoni wote tufurahi, umoja na mapendo katika Kristu

Wachungaji wote Jimboni, Umoja na mapendo katika Kristu

Na watawa wote jimboni, umoja na mapendo katika Kristu

Waamini wote jimboni, umoja na mapendo katika Kristu

Njoni sasa tufanye sherehe, umoja na mapendo katika Kristu.

MBELE YA KANISA KUU

Askofu anawaamkia watu akisema:

Neema na Amani viwe nanyi nyote katika kanisa la Mungu.

Wote: **Viwe pia nawe**.

Askofu: Ndugu wapendwa, tukishangilia tumefika hapa ili kutabaruku kanisa jipya kwa ajili ya adhimosho la sadaka ya Bwana. Tushiriki katika Neno la Mungu kwa imani, ili jumuiya yetu, iliyozaliwa upya, katika chemchemi moja ya ubatizo, na kulishwa kwa meza moja iongezeke na kuw hekalu la kiroho, na iongozwa kwa upendo wa juu, ikiwa imekusanyika kwenye altare moja.

Baada ya kufungua mlango, Askofu anawaalika watu, kwa maneno haya yafuatayo;

SEHEMU YA NNE

LITURUJIA YA EKARISTI.

TWENDE NA SADAKA (BY A. F. MUYONGA)

Twende na sadaka (kwake bwana) twende na sadaka zetu kwake (kwake Bwana) kwake Bwana muumba wetu.x2

Tuandamane kwa furaha tukicheza tukiwa tumeshika fedha zetu na tukiimba nyimbo twende tupeleke sadaka zetu x 2

1. Muda unapofika tusianze kufikiri fikiri tuinuke twende tu kampe Bwana mali yake
2. Bwana ndiye anayetupatia vitu tulivyo navyo tuinuke twende tukampe Bwana mali yake.

WAAMINI TUWE NA JUHUDI *(By J. NGANDU)*

Waamini tuwe na juhudi kulijenga Kanisa letu x2

Tutoe ukarimu, sehemu ya mali yetu aliyotujalia Mwenyezi Mungu x2

1. Waamiani tuwe tayari daima kujitolea kwa mali na kwa ukarimu sote tujenge Kanisa letu
2. Waanini amkeni tuwajibike kuinua hekalu la Mungu ndiyo nyumba ya sala na ibaada takatifu.
3. Kanisa litajengwa na sisi wenyewe nguvu kwa hiyo waanimi tufanye juhudi totoe michango yetu.

NAILETA SADAKA (BY H. MSIGWA - Geita Parish)

Naileta sadaka yangu kwa moyo ulioradhi na wenye upendo naomba upokee x 2

Ninaleta kwa upendo na kwaya moyo wa ukarimu na kwa moy waunyenyekevu

Ninajusihi Baba pokea sadaka yangu x2

1. Mazao ya mashamba ninaleta upokee ni juhudi zetu sisi

2. Nitasujudu nikilikabili hekalu lako takatifu nutalishukuru jina jina lako

Wimbo
MALAIKA MTAKATIFU (BY E. F. KIDALUSO)
Malaika mtakatifu amesimama kando ya altare akiwa ameshika mkononi chetezo cha dhahabu x2
Eee..... Bwana nakuomba sala yangua ipae kwako kama moshi wa ubani uipokee sadaka yangu nikutoleayo x2

KUWASHA MISHUMAA YA ALTARE NA TAA ZA KANISA.

Kisha kufukiza baadhi ya wahudumu wapanguse meza ya altare kwa vitambaa, na ikitakiwa waifunike kitambaa kisichopitisha maji.
Kisha wafunike altare vitambaa, na ikifaa waipambe kwa maua
Waweke mishukaa itakiwayo kwa adhimisho la Misa, na ikitakiwa waweke msalaba mahali pafaapo.

Kisha shemasi amwendee Askofu ambaye amesimama na amkabidhi mshumaa mdogo uwakao akisema kwa sauti.

Mwanga wa Kristo uangaze katika Kanisa,
ili uyafikishe mataifa yote kwenye kweli yote.

Kuwasha mianga ya sherehe kwafanyika hivi: mishumaa yote mishumaa iliyosimikwa ilipofanyika mipango, taa nyinginezo za kanisani kama ishara ya furaha kubwa huwashwa. Wakati huo huo antifona yaimbwa.

MWANGA WA KRISTO (BY NGURUMO A.)
Mwanga wa Kristu, mwanga wa Kristu, mwanga wa Kristu utuangaze.
Giza ondoa, giza ondoa, giza ondoa utuangaze
Tukutambue, tukutambue, tukutambue utuangaze

Ingieni kwa malango ya milele,
Mfalme wa utukufu apate kuingia.

NYIMBO ZA KUANDAMANA KUINGIA KANISANI

INGIENI HEKALUNI *(By Hilari Msigwa Geita Parish).*
Ingieni hekaluni mwa Bwana ili tukamsujudie Bwana jongeeni madhabahu ya Bwana ili tumwabudu.
Nyumba yake ni nyumba takatifu, mahali pa kumtolea sala, jongeeni patakatifu pake ili tumwabudu
Njooni nyumbani mwa Bwana Mungu x5 tumwabudu.

1. Nyumbani kwa Bwana Mungu mna neema tele tuingie kwa Shangwe tukamwabudu.

2. Nyua zake Bwana Mungu zapendeza sana, twende

NYUMBA YA MUNGU (ByVianney . S. Gallus, Mwangika Parish)
Nyumba ya Mungu imejengwa imara x2
(msingi wake upo juu ya mlima mtakatifu, nyuma imejengwa juu ya mwamba thabiti) x2

1.Hii ni nyumba ya Bwana, imejengwa kikamilifu juu ya mwamba imara, juu ya mwamba dhabiti
2.Nalifurahi waliponiambia twende waliponiambia na twende nyumbani kwake Bwana.

BARAKA YA MAJI NA KUNYUNYIZA.

Katika baraka hii Askofu anawaalika watu kwa maneno haya:

Ndugu wapendwa, tumwombe na kumusihi Bwana Mungu wetu tunapotabaruku nyumba hii kwa shangwe, apende kukibariki kiumbe hiki cha maji ambayo tutanyunyiziwa iwe alama ya toba na ukumbusho na ubatizo na zioshwe kuta mpya na altare mpya. Na Bwana mwenyewe atusaidie kwa neema yake ubaki wasikivu kwa roho tuliyempokea, na waaminifu katika Kanisa lake.

Wote wakae kimya wakisali kwa kitambo. Halafu Askofu anaendelea

Ee Mungu, kwa njia yako kila kiumbe kinafikia nuru ya uzima, na unawazungushia watu wote upendo mkubwa hivi ili wasilelewe tu kwa tunzo lako kibaba bali huwasafisha pia dhambi kwa umande wa wa mapendo, na kuwarudisha siku zote kwa Kristo, aliye kichwa chao.
Maana kwa shauri lako huruma ulipanga ili watu walioshuka katika kisima cha maji kama wenye dhambi, wafu pamoja na Kristo wakapande wakiwa wametakaswa wawe viomngo vyake, na wawe warithi wa tuzo za milele pamoja naye basi tutakatifuze kiumbe hiki cha maji kwa baraka + yako ili yanaponyunyiziwa kwetu na kwa kuta za Kanisa, yawe alama ya kiosho kile cha wokovu ambacho kwa hicho tumeoshwa katika Kristo tukafanyika hekalu la Roho wako.

Na sisi pamoja na ndugu wote tutakao adhimisha mafumbo matakatifu katika Kanisa hili,utujalie kuifikia Yerusalemu ya mbinguni. Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.

Wote: **Amina.**

Askofu akisindikizwa na mashemasi ananyunyizia watu na kuta za kanisa

2. Tuingie nyumba ya Bwana, tutoe maombi
   Tuingie nyumba ya Bwana,tutoe shukrani (ndio...

MAHALI HAPA PANATISHA SANA (BY FRT. SIMEON MAYALA)
Mahali hapa panatisha, mahali hapa panatisha sana x2
Hekalu la Mungu ni nyumba ya sala, ndiyo patakatifu pa kutolea sadaka kwa Mungu ni mahali pa sala.

1. Hekalu la Mungu ni nyumba ya sala ni mahali pa kumwabudia Mungu wetu, njoni nyote tumwabudu Mungu wetu.
2. Hekalu la Mungu ndiyo patakatifu ni mahali pa kutolea sadaka jioni nyote tumwabudu Mungu wetu.
3. Njoni nyote tumwabudu Mungu wetu kwa maana ndiye Mungu wetu njoni nyote tumsifu Mungu wetu.]

MBINGUNI NI KITI CHA ENZI (BY OCTAVIAN MICHAEL)
Mbinguni ni kiti cha enzi na duniani ni mahali pa kuweka miguu yangu.

1. Nitajenga nyumba ya namna gani, ya namna gani?
2. Nitakutolea sadaka gani? Kukushukuru Ee Bwana?
3. Nitakuimbia nyimbo gani, kukusifu Ee Bwana?

KUFUKIZIA ALTARE NA KANISA
Askofu anatia ubani katika chombo akisema:

Sala hii Ifike mbele yako, ee Bwana, kama moshi wa ubani ; na jinsi nyumba hii inavyojaa harufu nzuri, na kanisa lako lijae harufu nzuri ya Kristo.

Wimbo
MOSHI WA UBANI (BY J. E. MANGE)
Moshi wa manukato wapaa mbele ya Bwana kutoka mkono wa malaika x2
1. Nitakushukuru kwa moyo wangu wote, mbele ya miungu nitakuimbia nitakuimbia zaburi.

wanao, ee Bwana, baada ya kuifia dhambi wazaliwe upya kwa ajili ya uzima wa milele.
Humo waamini wako, waliozunguka meza ya altare, waadhimishe kumbukumbu ya Paska wakashibishwe kwa Neno la Kristo na kwa mwili wake.
Kutoka humo matoleo ya sifa yenye furaha yaende juu, sauti za watu zikiunganika na nyimbo za Malaika, na sala ya kudumu kwa ajili ya wokovu wa watu zipae .
Humo maskini wakute huruma, wanaogandamizwa wapate uhuru wa kweli, watu wote wajivike hadhi ya kuwa wanao hadi wafikie kwa shangwe Yerusalemu iliyo juu.
Tunaomba hayo kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, Mwanao, anayeishi na kutawala nawe katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu, daima na milele.

Wote: **Amina**

MPAKO WA ALTARE NA KUTA ZA KANISA.

Askofu anasimama mbele ya altare na kusema kwa sauti:

Altare na nyumba tunayopaka kwa
Utumishi wetu, Bwana atakatifukuze
Kwa nguvu yake,
Viwe ishara zinazoonekana
Za fumbo la Kristo na Kanisa.

Nyimbo
TAZAMENI NYUMBA YA MUNGU.(By Richard Mloka)
Tazameni nyumba ya Bwana inavyopendeza
Tazameni nyumba ya Bwana inavyopendeza
Ndio makao ya Mungu wetu mfano wa hekalu la mbinguni x2

1. Nyumba yake ni takatifu twapata neema
   Nyumba yake nyumba ya sala twende kwa uchaji
   (ndio makao ya Mungu wetu mfano wa hekalu hekalu la Mbinguni)x2

Wimbo 1.
Nimeona maji (By M Moshi)
Nimeona maji yakitoka, nimeona maji yakitoka he-kaluni x2
Upande wa kuume, upande wa kuume, upande wa kuume
Aleluya x2
1. Na watu wote waliofikiwa, na maji hayo wameokoka, nao wamesema Aleluya.
2. Uninyunyizie maji, ninyunyizie kwa mrashi ili niwe mweupe kuliko theluji.
3. Atukuzwe Baba na Mwana na Roho Mtakatifu, kama mwanzo na sasa na milele. Amina.

Wimbo 2.

BWANA LIBARIKI KANISA (By Octavian B. M. Paokia ya Bikira Maria Afya ya Wagonjwa)
Bwana libariki Kanisa hili ambamo wana wako tutakusanyika kutoa maombi na kukusifu wewe

1.Baba, Baba Mungu mwenyezi tunakuomba Bwana libariki kanisa, Ee Mungu twakuomba
2.Wote watakao ingia katika nyumba hii uwajaze baraka na neema zako
3.Wote watakao ingia katika nyumba hiii wakuabudu muumba wetu
4 .Wote watakaoingia katika nyumba hii wakusifu kwa shangwe muumba wetu.

Baada ya kunyunyizia Askofu anarudi kwenye kiti chake hali amesimama, mikono imefungwa anasema

Mungu Baba wa huruma awemo katika nyumba hii ya sala na neema ya Roho Mtakatifu ilitakase hekalu la makao yake ndio sisi.

Wote: Amina

GLORIA (UTUKUFU)
Askofu: **Gloria in excelsis Deo**

Gloria In excelsis Deo / et in terra pax hominibus bonae volutatis. / Laudamus te, / benedicimus te, / adoramus te, / glorificamus te, / gratias agimus tibi propter magnam gloriam tuam, / Domine Deus, Rex caelestis, Deus Pater omnipotens. / Domine Deus, Agnus Dei, fillius Patris, /
Qui tollis peccata mundi, Miserere nobis. / Qui tollis peccata mundi, suscipe deprecationem nostram. / Qui sedes ad dexteram Patris, Miserere nobis. / Quoniam tu solu sanctus, / tu solus Dominus, / tu solus Altissimus, Juse Chrite, / cum Sancto Spiritu, in Gloria Dei Patris. / Amen.

Askofu: **Tuombe**
Ee Mungu Mwenyezi wa milele, upamwagie mahali hapa neema yako, na uwagawie wote wanaokuomba tunu ya msaada wako, ili hapa nguvu ya N eno lako na mafumbo yako iimarishe mioyo ya waamini wote. Tunaomba hayo kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo Mwanao, anayeishi na kutawala nawe katika umoja wa Roho Mtakatifu, Mungu daima na milele.

Wote: **Amina**

SEHEMU YA PILI

LITURUJIA Y A NENO

Maandamano ya kuleta Neno la Mungu (Kama yatakuwepo)
(Shemasi na watumikizi wenye taa)

NENO LAKO NI TAA (R. MABANHU)
Neno lako ni taa ya miguu yangu miguu yangu x2
Neno lako ni taa ya miguu yangu
Neno lako ni mwanga wa njia yangu.
Neno lako ni nuru na uzima wangu.

1. Sheria yako naipenda ajabu, naitafakari mchana kutwa.
2. Mawazo yako huvuta hekama, kuliko adui zangu siku zote
3. Mausia yako ni matamu, kuliko asali kinywani mwangu

Katika altare ya Mungu mmepokea baraka
Ee watakatifu wa Mungu mtuombee kwa Bwana wetu Yesu Kristu.

1. Bwana ni nani atakayekaa katika hema yako, ni nani atakayefanya maskani yake katika Mlima wako mtakatifu
2. Ni mtu aendaye kwa ukamilifu na kutenda haki asemaye kweli kwa moyo wote.
3. Asiyesingizia kwa ulimi wake wala hakumtenda mwenziwe mabaya wala hakumsengenya jirani yake

Sala rasmi ya kutabaruku.

Ee Mungu Mwenyezi unayetakasa na kuongoza Kanisa lako, yatupasa kuadhimisha Jina lako kwa mbiu ya shangwe. Kwa sababu leo taifa la waaamini latarajia kutabarukiwa kwa shangwe nyumba hii ya sala, ambalo linakuheshimu kwa moyo, linalelewa kwa Neno na kulishwa kwa sakramenti. Majengo haya yadokeze fumbo la Kanisa, Kristo alilolitakasa kwa damu yake ili alifanye na kuonesha, Bi arusi wake mtukufu
Bikira anayeng'aa utimilifu wa imani, mama mwenye kutunza kwa uwezo wa Roho.
Kanisa takatifu, shamba la mizabibu teule la Bwana, ambalo matawi yake yaujaza ulimwengu wote, linalonyosha mpaka ufalme wa mbinguni machipukizi yake yaliyotengenezwa na mti.
Kanisa lenye heri , maskani yake Mungu na watu , hekalu takatifu, lililoijengwa kwa mawe hai katika misingi ya Mitume, Kristo Yesu akiwa jiwe kuu la pembeni.
Kanisa la juu, Mji uliojengwa katika kilele cha mlima, linaloonekana kwa wote, linalong'aa mbele ya wote, ambamo taa ya mwanakondoo yang'aa milele,na wimbo wa shukrani wa wenye heri wavuma.
Basi tunakuomba na kukusihi, ee Bwana: upende kutakatifuza kabisa kutoka mbinguni, kanisa hili na altare hii ili idumu daima kwa mahali patakatifu na meza iliyoandaliwa tayari siku zote kwa ajili ya sadaka ya Kristo.
Humo wimbi la neema ya Mungu lifunike makosa ya watu, ili

Kwa kufa na kufufuka kwako, utuokoe, Bwana
Kwa kumpeleka Rohao Matakatifu utuokoe, Bwana
Sisi wakosefu twakuomba, utusikie
Upende kulisimamia na kulilinda
Kanisa lako takatifu twakuomba, utusikie
Upende kumlinda Baba Mtakatifu na wote wenye
daraja katika Kanisa lako Takatifu twakuomba, utusikie
Upende kuwajalia mataifa yote amani
na mapendo ya kweli twakuomba, utusikie
Upende kutudhibitisha sisi na kutudumisha
katika utumishi wakomtakatifu twakuomba, utusikie
Upende kulitaksa Kanisa hili,
Yesu mwana wa Mungu aliye hai, twakuomba, utusikie
Kristo utusikie.
Kristo utusikie.
Kristo utusikilize.
Kristo utusikilize.

Baada ya kumaliza kuimba litania, Askofu amesisima, hali amepanua mikono asema:

Tunakuomba ee Bwana kwa hisani yako uyapokee maombi yetu,
Kwa ajili ya mombezi ya Bikira Maria Mwenye heri na ya watakatifu wote, ili majengo haya yatakayotabarukiwa kwa jina lako yafanywe nyumba ya wokovu na ya neema ambamo taifa la Wakristo, likikusanyika pamoja, likuabudu wewe katika roho na kweli na likajijenge katika upendo. Kwa njia ya Kristo Bwana wetu.

Wote: **Amina.**

KUZIKA MASALIO

Baadaye, ikiwa masalio ya mashahidi au watakatifu wengine yatazikwa katika altare, Askofu anaiendea altare. Shemasi au Padre anamletea Askofu masalio.

Wimbo:
KATIKA ALTARE YA MUNGU (By Octavian Michael)

Askofu anapokea kitabu cha masomo na kuwaonyesha watu akisema
Neno la Mungu livume siku zote katika ukumbi huu, mkafumbuliwe fumbo la Kristo
Nalo litende kazi katika Kanisa kwa ajili ya wokovu wenu.

Wote wajibu: **Amina**

SOMO LA KWANZA
Nehemia 8:1- 4a, 8-10

Na watu wote wakakusanyika kama mtu mmoja katika uwanja uliokuwa mbele ya lango la mji; wakmwambia Ezra, mwandishi, akilete kitabu cha torati ya Musa, Bwana aliyowaamuru Israeli. Naye Ezra kuhani, akileta torati mbele ya kusanyiko, la wanaume na wanawake, na wote walioweza kusikia na kufahamu, siku ya kwanza ya mwezi wa saba.

Akasoma humo mbele ya uwanja uliokuwa ukikabili lango la mji, tangu mapambazuko hata adhuhuri, mbele ya hao wanaume na wanawake, na wale walioweza kufahamu; na masikio ya watu wote yakasikiliza kitabu cha torati.

Naye Ezra kuhani, akasimama juu ya mimbari ya mti waliyokuwa wameifanya kwa kusudi hilo.

Nao wakasoma katika kitabu, katika torati ya Mungu, kwa sauti ya kusikilika; wakaeleza maana yake hata wakyafahamu yote.

Naye Nehemia, ndiye aliyekuwa Tirshatha, na Ezra kuhani, mwandishi na Walawi waliowafundisha watu, wakawaambia watu wote, “Siku hii ni takatifu kwa Bwana, Mungu wenu msiomboleze wala msilie.” Maana watu wote walilia wali-

poyasikia maneno ya torati. Kisha akawaambia, “ Enendeni zenu mle kilichonona, na kunywa kilicho kitamu, tena mpelekeeni sehemu yeye asiyewekewa kitu, maana siku hii ni takatifu kwa Bwana wetu; wala msihuzunike, kwa kuwa furaha ya Bwana ni nguvu zenu.”

Msomaji: Hilo ndilo Neno la Bwana.
Wote: Tumshukuru Mungu

Wimbo wa katikati

NALIFURAHI WALIPONIAMBIA ***(By FAN)***
Nalifurahi waliponiambia tutaingia nyumbani mwa Bwana
(miguu yetu imesimama ndani ya malango yako Ee Yerusalemu) x2
Amani iwe ndani ya ngome zako Na salama ndani ya nyumba zako.
(Miguu yetu imesimama ndani ya malango yako Ee Yerusalemu) x 2

(Mabeti yasomwe)
1. Sheria ya Bwana ni kamilifu huiburudisha nafsi.
   Ushuhuda wa Bwana ni amini humtia mjinga hekima
   Maagizo ya Bwana ni ya adili huufurahisha moyo.
   Amri ya Bwana ni safi huyatia macho nuru ***(Kiitikio)***
2. Kicho cha Bwana ni kitakatifu kinadumu milele
   Hukumu za Bwana ni kweli zina haki kabisa,
   Ni za kutamanika kuliko dhahabu, kuliko wingi wa dhahabu safi,
   Nazo ni tamu kuliko asali kuliko sega la asali. ***(Kiitikio)***
3. Maneno ya kinywa changu, na mawazo ya moyo wangu,
   Yapate kibali mbele zako, Ee Bwana, mwamba wangu na mwokozi wangu. ***(Kiitikio)***

Mtakatifu Mikaeli, utuombee
Watakatifu Malaika wa Mungu, utuombee
Mtakatifu Yohana Mbatizaji utuombee
Mtakatifu Yosefu utuombee
Watakatifu Petro na Paulo, mtuombee
Mtakatifu Adrea utuombee
Mtakatifu Yohane utuombee
Mtakatifu Maria Magdalena utuombee
Mtakatifu Stefano utuombee
Mtakatifu Inyasi wa Antiokia utuombee
Mtakatifu Laurenti utuombee

Mtakatifu Perepetua na Felista utuombee
Mtakatifu Anyesi utuombee
Mtakatifu Gregori, utuombee
Mtakatifu Augustino utuombee
Mtakatifu Atanasi utuombee
Mtakatifu Basili utuombee
Mtakatifu Martini utuombee
Mtakatifu Benedikto utuombee
Mtakatifu Francisko na Dominiko mtuombee
Mtakatifu Francisko (Xaveri) utuombee
Mtakatifu Yohane Maria (Viane) utuombee
Mtakatifu Katarina wa Siena utuombee
Mtakatifu Teresa wa Avila utuombee
Mtakatifu Karoli Lwanga na wenzake mtuombee
Mtakatifu Yosefina Bakhita utuombee
Mwenye heri Clementina Nangapeta Anuarite utuombee
Mwenye heri Victoria Rosoamanarivo utuombee
Mwenye heri Yosefu Gerardo utuombee
Mwenye heri Mama Theresa wa Kalkuta utuombee
Watakatifu wote wa Mungu mtuombee
Uturehemie utuokoe, Bwana
Katika uovu wowote utuokoe, Bwana
Katika dhambi yoyote utuokoe, Bwana
Katika mauti ya milele utuokoe, Bwana
Kwa kujifanaya mwanadamu, utuokoe, Bwana

SOMO LA PILI
1 Kor. 3: 9 – 13, 16-17

Ninyi ni jengo la Mungu. Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, niliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anvyojenga juu yake. Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipo-kuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristu. Lakini kama mtu akijenge juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani, au miti au majani, au manyasi, kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri. Maana siku ile itaidhihirisha, kwa kuwa yafunuliwa katika moto; na ule moto wenyewe utai-jaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani.

Hamjui kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu, Mungu atamharibu mtu huyo. Kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu ambalo ndilo ninyi.

Hilo ndilo neno la Bwana.

SHANGILIO *(J. MGANDU)*
Aleluya, Aleluya, Aleluya

Bwana asema hivi, mbinguni ni kiti changu cha enzi na duniani ni mahali pa kuweka miguu, miguu yangu, nita-jenga nyumba ya nama gani?

INJILI
Yoh. 2:13 – 22

Pasaka ya Wayahudi ilikuwa karibu; naye Yesu

alikwea mpaka Yerusalemu. Akaona pale hekaluni watu waliokuwa wakiuza ng'ombe na kondoo na njiwa, na wenye kuvunja fedha wameketi. Akafanya kikoto cha kambaa, akawatoa wote katika hekalu, na kondoo na ng'ombe; akamwaga fedha za wenye kuvunja fedha, akazipindua meza zao; akawaambia wale waliokuwa wakiuza njiwa, "Yaondoeni haya; msiifanye nyumba ya Baba yangu kuwa nyumba ya biashara". Wanafunzi wake wakakumbuka ya kuwa imeandikwa, Wivu wa nyumba yako utanila.

Hilo ndilo Neno la Bwana.
Wote: Sifa kwako Ee Kristu
Baada ya Homilia kanuni ya Imani Inasemwa

SALA RASMI YA KUTABARUKU NA MPAKO

Litania la watakatifu

Halafu Askofu anawaalika watu kusali kwa maneno, haya au yafananayo:

Wapendwa wote tumwombe Mungu Baba Mwenyezi , anayejifanyia mioyo ya waamini iwe hekalu la Kiroho na maombezi ya kindugu ya watakatifu yaunganike na sauti zetu.

Shemasi anawaalika waamini kwa kusema:
Tupige magoti.

Waimbaji	**wote**
Bwana uhurumie.	
Kristo utuhurumie,	
Bwana uhurumie.	
Maria mtakatifu, mama wa Mungu,	utuombee